

# MAELEKEZO YA MATUMIZI YA AQUASAFE™

Kadi ya Nasaha



## **KWA MAJI YALIYOTEKWA KUTOKA BILULA**



Weka kidonge 1 cha Aquasafe katika lita 20 za maji yasiyoonyesha uchafu



Subiri kwa dakika 30



Maji yako ya kunywa sasa ni salama na tayari

---



## **KWA MAJI YALIYOTEKWA KUTOKA MTO, KISIMA AU BWAWA**

(Maji yaliyotekwa kutoka mto, kisima au bwawa ni machafu zaidi kuliko maji ya bilula)



Weka vidonge 2 vya Aquasafe katika lita 20 za maji yasiyoonyesha uchafu



Subiri kwa dakika 30



Maji yako ya kunywa sasa ni salama na tayari

---



## **IKIWA MAJI YANAONEKANA KUWA NI MACHAFU AU YENYE TOPE**

Kwanza kabisa, chuja maji kwa kutumia kitambaa safi, kisha uweke vidonge 2 katika lita 20 za maji na usubiri kwa dakika 30 kabla ya kunywa maji hayo

**Kumbuka:** Maji yaliyosafishwa kwa kutumia Aquasafe ambayo yamehifadhiwa katika chombo chenye shingo nyembamba ambacho kina kifuniko kilichokazwa yanakuwa salama kunywa kwa muda hadi siku saba. Maji yaliyosafishwa ambayo yamehifadhiwa katika chombo chenye tundu pana au ambacho hakina kifuniko kilichokazwa ni salama kunywa kwa muda wa masaa 24 tu.